# Wafugaji wakimbilia nchi jirani kuuza mifugo kisa maslahi

Imetoka Ukurasa 1

zo la kupata malighafi itokanayo na mifugo, akidai kuwa wafugaji wanasema huko ina bei ya juu kuliko hapa nchini.

Gekul alikwenda kutembelea na kukagua kiwanda hicho na kusikiliza taarifa ya uendeshaji wake.

"Hiki kiwanda kimeanza uzalishaji tayari na kina uwezo wa kuchinja mbuzi 2,000 kwa siku na ng'ombe 500. Kimsingi, tumejipanga kuhakikisha kuwa wanafanya vizuri katika Bara la Afrika, kwa kuhakikisha tunasafirisha nyama kwa wingi nje, zenye viwango na ubora wa kimataifa," alisema Virjee.

Baada ya taarifa hiyo, Naibu Waziri huyo alisema kuanzia sasa ni vyema wafugaji wakawa wazalendo, kwa kuuza mifugo yao kiwandani hapo, kwa kuwa uchakataji wa mazao hayo yanafanyika hapa nchini na faida nyingi zinakuwa kwa ajili ya kunufaisha taifa na kuingiza fedha za kigeni.

"Wafugaji ifike mahali sasa, tuwe wazalendo kwa kuuza mifugo hapa nchini na ifike mahali tujisikie vibaya kunufaisha watu wengine au taifa lingine. Mifugo itoke Tanzania iende kunufaisha Kenya, ichakatwe Kenya, faida yote iende huko ndugu zangu hapa hatumuungi mkono, maana kwa matendo haya kiwanda kinakosa malighafi," alisema Gekul.

Aidha, kuhusu wingi wa tozo, Naibu Waziri huyo alisema amelichukua na kuahidi kuwa wizara yake chini ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, watakaa pamoja Wizara ya Fedha na Mipango na kutengeneza mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji hao. Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema kuwa kiwanda hicho ni mkombozi kwa wafugaji wa mikoa ya kanda ya kaskazini na mikoa ya jirani, kwa kuwa wafugaji watapata soko la uhakika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Dk. Jumaa Mhina, alisema watumishi wa serikali ya wilaya hiyo, wamefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wawekezaji hao kuhakikisha kiwanda hicho kinapatikana

Scanned with CamScanner

pa 29, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# Wafugaji wakimbilia nchi jirani kuuza mifugo kisa maslahi

Na Woinde Shizza, LONGIDO

MWEKEZAJI wa kiwanda cha kuchakata nyama cha Eliya Food Overseas Ltd kilichopo Wilaya ya Longido mkoani Arusha, amesema hali ya kibiashara kwa sekta hiyo si ya kuridhisha, kwa kuwa wafugaji wengi wanakimbilia kuuza mifugo yao nchi jirani kutokana na maslahi ya bei.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Irthan Virjee, alimweleza jana, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, kwamba bado wanakabiliwa na tati-

Inaendelea Uk. iii

Scanned with CamScanner

NIONAVYO

Na Mwandishi Wetu

# Ombi la wawekezaji kuomba serikali ipitie upya tozo ya mifugo ni suala la msingi

MKURUGENZI wa kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo cha Eliya Food Overseas, Shabbir Virjee ameiomba Serikali kuona uwezekano wa kupitia upya na kupunguza kodi na tozo za mifugo ili waweze kushindana vyema katika soko la Kimataifa na nchi jirani kama Ethiopia, Kenya, Somalia na Uganda ambazo kodi zao ni ndogo na zinawawezesha kununua na kuuza mifugo pamoja na mazao yake kwa bei nzuri.

Ombi hilo lilitolewa kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul alipotembelea kuona shughuli zinazofanywa katika kiwanda hicho cha kuchakata mazao ya mifugo kilichopo katika Kijiji cha Namanga Mpakani, Wilayani Longido, koani Arusha.

Wamesema kwa sasa wanalipa kodi zisizopungua tano kabla ya kusafirisha mazao ya mifugo nje ya nchi, jambo ambalo alisema limekuwa linawafanya wasiweze kushindana vizuri katika soko, kwa sababu ya bei yao kuwa juu kutokana na kodi wanazolipa hapa nchini.

Bila shaka kuna changamoto nyingi zinazowakabili wawekezaji sekta ya mifugo, lakini ni baadhi tu wameeleza, na ipo haja ya wawekezaji hao maombi yao kutekelezwa kikamilifu.

Wanasema changamoto nayowakabili ni kodi, kulipa kodi zisizopungua tano kwa Wizara ya Kilimo shilingi 50 kwa kila.

Mbali kodi hiyo pia wanalipa Bodi ya Nyama asilimia 1 ya thamani, Bakwata wanalipa kwa ajili ya kibali cha Halal, tunalipa kodi kwa Vibali vingine.

Pia wanalipa asilimia 0.1 ya kodi ya mionzi, kila hatua wanalipa kodi ambazo kusema ukweli zinawafanya kushindwa kushindana na nchi jirani ambazo kodi zao ni ndogo.

Pia changamoto nyingine wanayokutana nayo ni kutopatikana kwa wanyama kama malighafi katika kiwanda hicho huku wakiomba Serikali kuwasaidia ili waweze kupata Wanyama wengi ili kiwanda kiwe na uhakika wa malighafi.

"Mhe. Waziri tunachangamoto nyingine ya kupata wanyama kama malighafi hapa kiwandani, Wafugaji wengi wanakwenda kuuza mifugo yao nchini Kenya kwa sababu ya bei nzuri huko, tunaomba tusaidiwe ili tuweze kupata malighafi ya uhakika, sisi hapa tunachinja kwa siku Mbuzi 2000 na Ngombe 400 hivyo unaweza kuona kuwa tunahitaji mkubwa wa kuwa na uhakika wa malighafi ya kutosha kila siku," alisema mkurugenzi wa kiwanda hicho Shabbir Virjee.

> **Wawekezaji sekta ya mifugo wanasema wanalipa kodi zisizopungua tano kabla ya kusafirisha mazao ya mifugo nje ya nchi, hali ambayo mmojawao anasema kwamba imekuwa ikisababisha wasiweze kushindana vizuri katika soko, sababu bei zao huwa ni kubwa kutokana na kodi wanazolipia hapa nchini**
>
> ***

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kama hali itaendelea hivyo uendeshaji wa kiwanda hicho utakuwa mgumu kwa sababu watashindwa kushindana katika soko la ndani hata nje, huku akisema lengo la kiwanda hicho ni kutoa ajira kwa Watanzania wasiopungua 150.

Mbali na kukabiliwa na changamoto hizo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul aliwapongeza wawekezaji hao kwa jitihada kubwa walizozifanya kuwekeza kiwanda hicho ambacho kinatekeleza adhma ya Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ya kuona Tanzania inakuwa nchi ya Viwanda na aliwahakikishia changamoto zao amezichukua na zitafanyiwa kazi.

"Nakuagiza Katibu Mkuu, Prof. Gabriel uunde timu itakayokuja kufuatilia ili kubaini hizo changamoto zote ikiwemo kwa nini Wafugaji wanapeleka mifugo yao kuuza nje ya nchi na taarifa hiyo ifike haraka ili tuweze kuishauri serikali kutatua changamoto hizo mapema," alisema Gekul.

Pia, Waziri Gekul alimuagiza Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel kuangalia kwa namna gani Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inavyoweza kusaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa malighafi katika kiwanda hicho.

"Hiki kiwanda ni lazima tukilinde, tufanye kila linalowezekana kukilinda kiwanda hiki, ikiwemo kutoa elimu kwa wafugaji kujua uwepo wa kiwanda hiki na faida zake, ili waweze kujua kumbe wanaweza kuuza ng'ombe wao hapa hapa nchini bila kukimbilia nchi nyingine," alisema Gekul.

Alisema wizara itaendelea kuwawezesha wafugaji kupitia vituo vya uhimilishaji hapa nchini kuwapata mbegu bora zitakazowasaidia kupata ng'ombe wazuri watakao wawezesha kupata kipato kizuri kupitia viwanda vinavyochakata mazao ya mifugo nchini.

Tangu Kiwanda hicho kianze kufanya kazi miezi miwili iliyopita wameshachinja Mbuzi zaidi ya 7000 na wameshaanza kupata masoko ya Kimataifa Uarabuni, Oman, Saudi Arabia na wanaendelea kufuatilia soko katika nchi ya China.

Nionavyo ni vyema sasa serikali ikawapunguzia changamoto wanazokabiliwa nazo ili waweze kusonga mbele kimaendeleo.

Mbali ya kampuni hiyo kupata mafanikio pia naamini Watanzania watapata ajira kutokana na sekta hiyo.

Mpango wa Serikali ni kufikia uchumi wa viwanda 2025 hivyo ni vyema ngumu ya usimamizi wa viwanda kama hivyo ukawa makini.

Scanned with CamScanner